**Kuingia هَمْزَةُ الْوَصْلِ (Hamzatul-waswl) Katika هَمْزَةُ الْقَطْعِ (Hamzatul-Qatw') Katika Neno Moja:**

Maneno yanayokutana pamoja هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl) na هَمْزَةُ الْقَطْعِ (hamzatul-qatw') ni machache katika Qur-aan. Yanaposomwa pekee au yanapoanziwa kusomwa, هَمْزَةُ الْقَطْعِ (hamzatul-qatw') ambayo ina sukuwn hubadilika kuwa ni ya madd hivyo husomwa kwa kuvuta harakah mbili:

| Linapoanza kutamkwa | Linapoungwa | Aayah |
|---|---|---|
| **uwtumina** | **...alladhi (+ sukuwn) tumina amaanatahu**<br><br>**Bonyeza usikilize** | فَلْيُؤَدِّ ٱلَّذِى ٱؤْتُمِنَ أَمَـٰنَتَهُۥ [1] |
| **iytinaa** | **...yaa Swaalihu (+ sukuwn) tinaa...**<br><br>**Bonyeza usikilize** | وَقَالُواْ يَـٰصَـٰلِحُ ٱئْتِنَا بِمَا تَعِدُنَآ [2] |
| **iydhan-liy** | **...may-yaquwlu (+ sukuwn) dhan-liy...**<br><br>**Bonyeza usikilize** | وَمِنْهُم مَّن يَقُولُ ٱئْذَن لِّى وَلَا تَفْتِنِّىٓ ۚ [3] |
| **iytuw** | **...thumma (+ sukuwn) tuw swaffaa** | فَأَجْمِعُواْ كَيْدَكُمْ ثُمَّ ٱئْتُواْ صَفًّا ۚ [4] |

[1]Al-Baqarah (2: 283)
[2]Al-A'raaf (7: 77)
[3]At-Tawbah (9: 49)
[4]Twaahaa (20 : 64)

| | | |
|---|---|---|
| | Bonyeza usikilize | |
| **iytuwniy (pekee)**<br><br>**(rejea juu)** | **...fis-samaawaati (+ sukuwn) tuwniy bikitaabin...**<br><br>Bonyeza usikilize | أَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِى ٱلسَّمَـٰوَٰتِ ۖ ٱئْتُونِى بِكِتَـٰبٍ مِّن قَبْلِ هَـٰذَآ [5] |

**Kuingia هَمْزَةُ الْقَطْعِ Hamzatul-Qatw' Katika هَمْزَةُ الْوَصْلِ Hamzatul-Waswl:**

Hutokea katika فِعْلٌ (kitenzi) na اسم (nomino)

**Katika فِعْلٌ (kitenzi)**

هَمْزَةُ الإِسْتِفْهام Hamzatul-istifhaam (hamzah ya kuuliza) ikiweko kabla ya هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl) hubatilishwa هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl) kwa maandishi na kwa kutamkwa, kisha هَمْزَةُ الإسْتِفْهام (hamzatul-istifhaam) ambayo ni هَمْزَةُ الْقَطْعِ (hamzatul-qatw') yenye fat-hah kwa kuwa ni ya إِسْتِفْهام(kuuliza), inabakia daima kutamkwa kwa fat-hah. Hii inapatikana katika Qur-aan katika hali saba zinazofuatia hapo chini. Maneno yaliyo katika rangi nyekundu ambayo ni vitenzi, yote asili yake yalikuwa na هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl) lakini kwa sababu ya هَمْزَةُ الْقَطْعِ (hamzatul-qatw') ambayo katika hali hii imegeuka kuwa ni ya إِسْتِفْهام (kuuliza), هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswli) imeondoshwa katika maandishi na katika matamshi, kwani *i'raab* ya هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl) katika vitenzi ni katika hali mbili tu; dhwammah au kasrah. Kwa hiyo bila shaka kuweko na fat-hah katika hali hii inadhihirisha kwamba Hamzah hiyo ni هَمْزَةُ الْقَطْعِ .

[5] Al-Ahqaaf (46: 4)

| Asili yake katika kuuliza | Aayah |
|---|---|
| أ + اِتَّخَذْتُم = أَتَّخَذْتُم | قُلْ أَتَّخَذْتُمْ عِندَ ٱللَّهِ عَهْدًا فَلَن يُخْلِفَ ٱللَّهُ عَهْدَهُۥٓ ۖ [6] |
| أ + اِطَّلَعَ = أَطَّلَعَ | أَطَّلَعَ ٱلْغَيْبَ أَمِ ٱتَّخَذَ عِندَ ٱلرَّحْمَٰنِ عَهْدًا ﴿٧٨﴾ [7] |
| أ + اِفْتَرَى = أَفْتَرَى | أَفْتَرَىٰ عَلَى ٱللَّهِ كَذِبًا أَم بِهِۦ جِنَّةٌۢ ۗ [8] |
| أ + اِصْطَفَى = أَصْطَفَى | أَصْطَفَى ٱلْبَنَاتِ عَلَى ٱلْبَنِينَ ﴿١٥٣﴾ [9] |
| أ + اِتَّخَذْنَاهُمْ = أَتَّخَذْنَاهُم | أَتَّخَذْنَٰهُمْ سِخْرِيًّا أَمْ زَاغَتْ عَنْهُمُ ٱلْأَبْصَٰرُ ﴿٦٣﴾ [10] |
| أ + اِسْتَكْبَرْتَ = أَسْتَكْبَرْتَ | أَسْتَكْبَرْتَ أَمْ كُنتَ مِنَ ٱلْعَالِينَ ﴿٧٥﴾ [11] |
| أ + اِسْتَغْفَرْتَ = أَسْتَغْفَرْتَ | سَوَآءٌ عَلَيْهِمْ أَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ أَمْ لَمْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ [12] |

.

**Katika** اسم **(nomino)**

هَمْزَةُ الإِسْتِفْهامِ (Hamzah ya kuuliza) ikiweko katika nomino ambayo ina لامُ التَّعْرِيفِ (laamut-ta'riyf - laam ya kibainishi), hamzah zote hubakishwa na kusomwa kwa hukmu ya المدُّ الْكَلمَيّ (al-maddul-kalimiyy[13]) ambayo ni kuvuta haraka sita. Hii inapatikana katika Qur-aan kwenye maneno matatu pekee katika Aayah sita zifuatazo:

---

[6]Al-Baqarah (2: 80)
[7]Maryam (19: 78)
[8]Sabaa (34: 8)
[9]As-Swaffaat (37: 153)
[10]Swaad (38: 63)
[11]Swaad (38: 75)
[12]Al-Munaafiquwn (63: 6)
[13] Rejea mlango wa 'al-madd al-laazim al-kalimiyy al-muthaqqal' na 'al-madd al-laazim al-kalimiyy al-mukhaffaf'.

| Inavyotamkwa | Asili yake katika kuuliza | Aayah |
|---|---|---|
| AaaaaaaLLahu<br><br>Bonyeza usikilize | أ + اللّٰه =<br><br>ءَآللَّهُ | قُلْ ءَآللَّهُ أَذِنَ لَكُمْ ۖ [14]<br><br>ءَآللَّهُ خَيْرٌ أَمَّا يُشْرِكُونَ ۝٥٩ [15] |
| aaaaaaadh-dhakarayni<br><br>Bonyeza usikilize | أ + أَلذَّكَرَيْنِ =<br><br>ءَآلذَّكَرَيْنِ | قُلْ ءَآلذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ أَمِ ٱلْأُنثَيَيْنِ أَمَّا<br><br>ٱشْتَمَلَتْ عَلَيْهِ أَرْحَامُ ٱلْأُنثَيَيْنِ ۖ [16] |
| aaaaaal-aana<br><br>Bonyeza usikilize | أ + أَلْأَنَ =<br><br>ءَآلْـَٔـٰنَ | ءَآلْـَٔـٰنَ وَقَدْ كُنتُم بِهِۦ تَسْتَعْجِلُونَ ۝٥١<br>[17]<br><br>ءَآلْـَٔـٰنَ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ وَكُنتَ مِنَ<br><br>ٱلْمُفْسِدِينَ ۝٩١ [18] |

## هَمْزَةُ الْقَطْعِ Hamzatul-qatw' Inapokutana na هَمْزَةُ الْقَطْعِ Hamzatul-qatw'

Inapokutana هَمْزَةُ الْقَطْعِ na هَمْزَةُ الْقَطْعِ pamoja, yaani mara mbili, zote zinapasa kupewa haki yake kwa kutamkwa zote

يَقُولُونَ أَءِنَّا لَمَرْدُودُونَ فِى ٱلْحَافِرَةِ ۝١٠ أَءِذَا كُنَّا عِظَـٰمًا نَّخِرَةً ۝١١ [19]

---

[14]Yuwnus (10: 59)
[15]An-Naml (27: 59)
[16]Al-An'aam (6: 143- na 144)
[17]Yuwnus (10: 51)
[18]Yuwnus (10: 91)
[19]An-Naazi'aat (79: 10-11)

Neno la pekee katika Qur-aan kwa riwaayah ya Hafsw, ambalo هَمْزَةُ الْقَطْعِ ya pili husomwa kwa usahali katika kutamkwa, nalo limewekewa alama ya kiduara juu ya هَمْزَةُ الْقَطْعِ ya pili ni ءَاعْجَمِيٌّ linalopatikana katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

وَلَوْ جَعَلْنَٰهُ قُرْءَانًا أَعْجَمِيًّا لَّقَالُوا۟ لَوْلَا فُصِّلَتْ ءَايَٰتُهُۥٓ ۖ ءَا۬عْجَمِىٌّ وَعَرَبِىٌّ ۗ [20]

*... a'jamiyyun wa 'Arabiyyun*

**Bonyeza usikilize**

[20]Fusw-sswilat (41: 44)